



Unapojibu tafadhali taja;
Kumb. Na CDC/I.20/VOL 1/32

10/01/2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WAKUSANYA MAPATO VIJIJINI – NAFASI 112.
(REVENUE COLLECTORS)**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anawatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi ya kazi ya kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

1: SIFA ZA MUOMBAJI:

- i). Awe raia wa Tanzania
- ii). Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
- iii). Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- iv). Awe ni mkazi wa eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.
- v). Awe na mdhamini mwenye kiasi cha Fedha au mali isiyo hamishika yenye thamani ya kuanzia TZS 3,000,000/= (milioni tatu) na zaidi. Dhamana ya fedha italazimika kuwasilishwa Halmashauri kupitia akaunti ya amana. Dhamana ya mali isiyo hamishika itathibitishwa kwa kuwasilisha Halmashauri hati au nyaraka ya umiliki inayotambulika na iliyothibitishwa kisheria kuwa ni mali ya mtoa dhamana.
- vi). Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai au kuhukumiwa kifungo jela katika Mahakama yoyote.
- vii) Awe tayari kufanya kazi katika Kata na Vijiji vya Kata hiyo ili kupunguza gharama za malazi.
- viii) Mtu yeyote aliyewahi kufanya kazi na Halmashauri kisha kuisababishia hasara ya upotevu wa mapato au kudaiwa na halmashauri, **HARUHUSIWI KUOMBA**

KAZI YA KUKUSANYA MAPATO.

2. Namna ya kuomba:

- a. barua ya maombi ipite kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata.
- b. Barua iambatane na picha ya muombaji.

2: MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO:-

- i). Kukusanya mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo katika eneo la wilaya ya Chemba kwa kutumia mashine ya kielektroniki (POS).
- ii). Kuwasilisha benki kupitia akaunti ya mapato ya halmashauri makusanyo yote yaliyokusanywa ndani ya saa 24 katika siku za kazi au siku ya kwanza ya kazi ya wiki au baada ya sikukuu.
- iii). Kutoa risiti za mashine ya kielektroniki (POS) kiasi sawa na fedha atakayolipa mlipaji.
- iv). Kutunza vifaa vya kukusanyia mapato (POS, rejista) na nyaraka za benki au Halmashauri zinazothibitisha uingizaji wa fedha benki.
- v). Kufanya uhakiki kila siku wa makusanyo ya siku na taarifa ya mashine ya kukusanyia mapato.
- vi). Kuwasilisha Halmashauri mashine ya kukusanyia mapato (POS) kwa ajili ya Ukaguzi /uchunguzi.
- vii). Kufanya kazi zingine zinazohusu mapato kadri atakavyoelekezwa na Mwajiri.

3: MUDA WA AJIRA.

Ajira ya Mkataba ya miezi sita kuanzia mwezi Januari 2023 hadi Juni 2023.

Atakuwa chini ya uangalizi wa utendaji wa Kata na Kijiji husika.

Mkusanyaji ataongezewa mkataba kutokana na juhudi yake katika kukusanya mapato.


4: MALIPO YA MKUSANYA MAPATO:-

Malipo kwa kazi ya ukusanyaji mapato yatakuwa asilimia 5 (5%) ya makusanyo yaliyokusanywa na kuwasilishwa Benki.

Maombi yatumwe kwa:

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S. L. P. 830,
CHEMBA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 24/01/2023 saa 9.30 mchana.



SIWEMA H. JUMAA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

CHEMBA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
CHEMBA